# MFUKO WA MISITU TANZANIA

*Kwa Kudumisha Ugharimiaji*
*wa Usimamizi wa Misitu*

## *TANGAZO LA KUITISHA MAANDIKO YA MIRADI, MWAKA 2021*

### 1.0 UTANGULIZI

Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ni Mfuko wa Umma ulioanzishwa kisheria (chini ya Sheria ya Misitu Sura Na. 323), kama chanzo endelevu cha fedha kwa ajili ya kuwezesha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu hapa nchini. Mfuko huu upo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na unasimamiwa na Bodi ya Wadhamini. Mfuko wa Misitu Tanzania ulianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Julai 2011 na unafanya kazi katika Mikoa ya Tanzania Bara.

### 1.1 Majukumu ya Mfuko wa Misitu Tanzania

Majukumu ya Mfuko wa Misitu Tanzania yameainishwa katika kifungu cha 80 cha Sheria ya Misitu Sura Na. 323 kama ifuatavyo:

(i). Kuwezesha uhamasishaji Jamii kupitia elimu na mafunzo kuhusu umuhimu wa uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu;

(ii). Kuwezesha na kugharami uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa misitu kwa kutoa ruzuku kwa vikundi na wadau wengine wanaojihusisha na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu;

(iii). Kukuza, kuendeleza na kugharamia utafiti kwa lengo la kuboresha uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali misitu;

(iv). Kusaidia na kuiwezesha Tanzania kunufaika na mipango na misaada ya Kitaifa na Kimataifa iliyopo kwa ajili ya kuhifadhi na kulinda bioanuwai na kuendeleza rasilimali misitu;

(v). Kusaidia na kuwezesha vikundi na watu binafsi kushiriki katika mijadala na midahalo inayohusu misitu na kuandaa tathmini za kimazingira kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 18 cha Sheria ya Misitu Sura Na. 323;

(vi). Kusaidia na kuwezesha vikundi na watu binafsi ili wafuate Sheria ya Misitu, kanuni na miongozo husika; na

(vii). Kugharamia shughuli nyingine zinazoendana na majukumu ya Mfuko na shughuli zinazohusiana na madhumuni ya Sheria ya Misitu Sura Na. 323.

## 2.0 WITO WA KUWASILISHA MAANDIKO YA MIRADI KUOMBA RUZUKU

Mfuko wa Misitu Tanzania unashirikisha wadau katika kutekeleza majukumu yake ambapo utoaji wa ruzuku ni njia mojawapo ya ushirikishwaji. Kupitia tangazo hili, Mfuko wa Misitu Tanzania unaitisha Maandiko ya Miradi. Aidha, wadau wanajulishwa kuwa, kwa mwaka 2021 kipaumbele cha utoaji wa ruzuku kitakuwa ni miradi inayohusiana moja kwa moja na upandaji miti katika mikoa ya nyanda kame na miradi inayohusiana na uendelezaji wa sekta ndogo ya ufugaji nyuki. Shule za msingi na sekondari kutoka wilaya 18 za mikoa 8 ya nyanda kame, zitafikiriwa kupatiwa ruzuku kwa ajili ya kuanzisha vitalu vya miti na kushiriki katika upandaji wa miti katika maeneo yao. Shule zitakazofanikiwa kupatiwa ruzuku, zinategemewa kutoa hamasa ya upandaji miti katika shule na vijiji vya jirani.

## 3.0 WALENGWA (WANAOWEZA KUOMBA RUZUKU)

Maandiko ya miradi ya kuomba ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Misitu Tanzania yanakaribishwa kutoka kwa vikundi vya kijamii; asasi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu; jumuiya/taasisi za kidini; asasi/taasisi za mafunzo; shule za msingi na sekondari; taasisi za utafiti; Idara na Wakala za Serikali; Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali. Waombaji wa ruzuku wawe wanatekeleza shughuli zinazohusiana na uhifadhi na usimamizi wa misitu, ufugaji nyuki, na uendelezaji wa rasilimali misitu katika mikoa ya Tanzania. Aidha, vikundi/asasi/taasisi zote zitakazowasilisha maandiko ya miradi kwa ajili ya kuomba ruzuku ni lazima viwe/ziwe vime/zimesajiliwa na mamlaka zinazotambulika kisheria. Nakala/vivuli vya nyaraka (vyeti vya usajili) zinazothibitisha usajili wa vikundi/asasi/taasisi husika zinapaswa kuambatishwa kwenye maandiko ya miradi.

## 4.0 MAENEO YA KIPAUMBELE YATAKAYOZINGATIWA KATIKA UTOAJI WA RUZUKU

Mfuko wa Misitu Tanzania utatoa ruzuku katika maeneo matatu ya kipaumbele kama ifuatavyo:

4.1 Uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Kipaumbele katika utoaji wa ruzuku kwa mwaka 2021 ni miradi inayohusu:

(i) Uanzishwaji wa vitalu vya miti shuleni na upandaji miti katika shule za msingi na sekondari na vijiji vya jirani. Waombaji wa ruzuku katika eneo hili ni shule za msingi na sekondari na ruzuku itatolewa kwa shule za msingi na sekondari kutoka wilaya 18 za mikoa 8 ya nyanda kame ambayo ni **Dodoma** ***(Wilaya za Dodoma na Chamwino)***; **Singida** ***(Wilaya za Ikungi na Singida)***; **Shinyanga** ***(Wilaya za Shinyanga na Kishapu)***; **Simiyu** ***(Wilaya za Bariadi na Busega)***; **Manyara** ***(Wilaya za Babati na Hanang)***; **Arusha** ***(Wilaya za Arumeru, Monduli na Longido),*** **Kilimanjaro** ***(maeneo ya tambarare ya Wilaya za Rombo na Same)*** **na Kagera** ***(Wilaya za Biharamulo, Karagwe na Ngara),***.

(ii) Uanzishwaji wa mashamba madogo ya miti ya kupanda *(woodlots).* Ruzuku itatolewa kwa mikoa yote ya Tanzania bara isipokuwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Pwani na Dar es Salaam. Kigezo cha kupatiwa ruzuku kitakuwa jitihada za kupanda miti zilizooneshwa na mwombaji wa ruzuku na uwepo wa shamba linalomilikiwa kihalali na mwombaji wa ruzuku lenye ukubwa usiopungua ekari 10.

4.2 Uboreshaji wa maisha ya jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu ya hifadhi, hususani miradi inayohusiana na ufugaji nyuki inayolenga uhifadhi wa misitu. Maeneo ambayo yatafikiriwa kupatiwa ruzuku ni:

(i) Kuboresha uhifadhi wa misitu ya asili kupitia ufugaji nyuki katika **Mikoa ya Lindi, Mbeya, Songwe, Rukwa, Tabora, Shinyanga, Kigoma na Katavi.** Walengwa hapa ni vikundi vya ufugaji nyuki ambavyo vitapatiwa pia mafunzo ya kutengeneza mizinga bora ya nyuki. **Vikundi vya wanawake na vijana vitapewa kipaumbele**.

(ii) Uanzishwaji wa vituo vya ukusanyaji wa asali na mazao mengine ya nyuki katika mikoa ya **Katavi, Rukwa, Geita, Tabora, Kigoma, Singida, Lindi, Mbeya, na Songwe**. Walengwa hapa ni Taasisi za Serikali zikiwemo TFS na Halmashauri za Wilaya.

4.3 Utafiti wa Misitu na Nyuki unaolenga kuboresha uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu na nyuki na kuongeza thamani kwa mazao ya misitu na nyuki utafikiriwa kupatiwa ruzuku. Miradi ya utafiti itakayopatiwa ruzuku inapaswa kutokana na **Mpango Kabambe wa Taifa wa Utafiti wa Misitu** (***National Forest Research Master Plan) na*** **Mpango Kabambe wa Taifa wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki** (***National Beekeeping Research Master Plan).***

***Kwa mwaka 2021, waombaji wa ruzuku katika eneo la kipaumbele cha utafiti wa misitu na nyuki ndio pekee wanaoweza kutekeleza miradi katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Waombaji ruzuku katika maeneo mengine ya kipaumbele wanapaswa kuangalia mikoa iliyotajwa kwenye kipaumbele husika.***

## 5.0 AINA ZA RUZUKU ZINAZOTOLEWA NA MFUKO WA MISITU TANZANIA

Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa ruzuku za aina tatu ambazo ni kama ifuatavyo:

(i) **Ruzuku Ndogo:** kiasi cha fedha kisichozidi Shilingi za Kitanzania (TZS) milioni tano (5). Kwa mwaka 2021 ruzuku ndogo itatolewa kwa shule za msingi na sekondari kutoka wilaya 18 za mikoa 8 zilizotajwa kwenye kipengele namba 4.1 (i) hapo juu. **Aidha, kwa tangazo la mwaka 2021 ruzuku haitatolewa kwa makampuni na watu binafsi. Aidha, Wanachuo wanaosoma shahada ya uzamili *(Masters Degree)* na Uzamivu (PhD) wanaweza kuomba ruzuku ndogo kama watu binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya utafiti katika misitu na nyuki inayohusiana na maandiko ya utafiti wa masomo yao.**

(ii) **Ruzuku ya Kati:** kiasi cha fedha kinachozidi TZS milioni tano (5) lakini hakizidi TZS milioni 20. Ruzuku hii itatolewa kwa wadau waliotajwa kwenye kipengele Na. 3 isipokuwa shule za msingi na sekondari.

(iii) **Ruzuku Kubwa:** kiasi cha fedha kinachozidi TZS milioni 20 lakini hakizidi TZS milioni 50. Ruzuku hii itatolewa kwa wadau waliotajwa kwenye kipengele Na. 3 isipokuwa shule za msingi na sekondari.

**Mwongozo wa Kuandaa Maandiko ya Miradi na Utaratibu wa Kutoa Ruzuku wa Mfuko wa Misitu Tanzania, utazingatiwa katika utoaji wa ruzuku za aina zote*. Hata hivyo*, *kwa tangazo la mwaka 2021, makampuni na watu binafsi wanashauriwa kutowasilisha maombi ya ruzuku kwa kuwa hayatafikiriwa, isipokuwa kwa miradi ya ruzuku ndogo ya utafiti wa misitu na nyuki kama ilivyofafanuliwa kwenye kipengele namba 5 (i) hapo juu.***

## 6.0 AINA YA UWEZESHAJI UNAOTOLEWA NA MFUKO WA MISITU TANZANIA

Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa aina tatu za uwezeshaji kama ifuatavyo:

(i) **Uwezeshaji wa Fedha:** Waombaji wa ruzuku wanaweza kupatiwa fedha kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa kwenye maandiko yao ya miradi;

(ii) **Uwezeshaji wa Vifaa:** Waombaji wa ruzuku wanaweza kupatiwa vifaa kama vile nyenzo na vitendea kazi vilivyoainishwa kwenye maandiko yao ya miradi ; na

(iii) **Uwezeshaji wa Stadi/Utaalam**: Mfuko wa Misitu Tanzania utawezesha utoaji wa mafunzo ya muda mfupi, hususani mafunzo ya ufugaji nyuki, utengenezaji wa mizinga, uanzishwaji wa vitalu vya miti na upandaji miti.

## 7.0 VIGEZO VINAVYOTUMIKA WAKATI WA KUCHAGUA MIRADI ITAKAYOPATIWA RUZUKU

Maandiko ya miradi ambayo yatafikiriwa kupatiwa ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania yanapaswa kutimiza vigezo vifuatavyo. Andiko la mradi lioneshe /lithibitishe kuwa:

(i) utekelezaji wa mradi utachangia katika uhifadhi, usimamizi na/au uendelezaji wa rasilimali misitu;

(ii) mradi unatoa faida ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kwa walengwa;

(iii) shughuli zitakazotekelezwa zibainishwe wazi na kuonesha uwepo wa uwajibikaji;

(iv) kuna ubunifu na ushirikishwaji wa wadau;

(v) matokeo ya utekelezaji wa mradi yatachangia uboreshaji wa uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu;

(vi) uwezo wa mwombaji wa kutekeleza na kusimamia shughuli za mradi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa;

(vii) kuna uendelevu wa shughuli za mradi zitakazotekelezwa baada ya ukomo wa ruzuku;

(viii) waombaji wa ruzuku ya kati na ruzuku kubwa watachangia asilimia 20 (fedha au hali na mali) ya jumla ya fedha zote zinazoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania;

(ix) kuna watekelezaji mradi wenye ueledi wa aina ya mradi ulioombewa ruzuku kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wake;

(x) umiliki wa eneo litakalotumika kwa shughuli za mradi ubainishwe;

(xi) maandiko ya miradi ya shule za msingi na sekonadari lazima yanapaswa kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Halmashauri husika; na

(xii) miradi itatekelezwa katika Mikoa ya Tanzania Bara na izingatie mikoa ya kipaumbele iliyotajwa kwenye kipengele Na. 4.1; 4.2 na 4.3 hapo juu.

**Maandiko yote ya miradi ambayo yatafanana au yatakuwa na vipengele vinavyofanana hayatapatiwa ruzuku kwa kuwa ni vigumu kutofautisha andiko la mradi lililoandaliwa na andiko la mradi lililonakiliwa kutoka maandiko mengine.**

## 8.0 UWASILISHAJI WA MAANDIKO YA MIRADI

Kwa tangazo la mwaka 2021, waombaji wa ruzuku wanapaswa kuwasilisha maandiko ya miradi kwa njia mbili:

### 8.1 Kuomba Ruzuku kwa Kutumia Mfumo wa Kielektroniki *(MNRT Portal)*

Waombaji wa ruzuku kwa njia ya mtandao (*online application*) watatakiwa kujisajii kwenye mfumo wa **MNRT Portal** na kuwasilisha maandiko ya miradi kwa kutumia mfumo huo. Kufungua mfumo wa **MNRT Portal** tumia anwani *(link)* ifuatayo: **https://portal.maliasili.go.tz/** Atakayepata tatizo wakati wa kujisajili au wakati wa kuomba ruzuku kwa kutumia mtandao wa **MNRT Portal** anaombwa kuwasiliana na mtaalam wa TEHEMA kwa kupitia namba za simu zifuatazo: **0684 004 855** au **0754 043 280.**

Waombaji wa ruzuku watakaowasilisha maandiko ya miradi kwa kutumia mtandao wa **MNRT Portal** watapokea ujumbe kwenye simu zao wa kuwajulisha kuhusu kupokelewa kwa maandiko yao ya miradi.

### 8.2 Kuwasilisha Maandiko ya Miradi kwa njia ya Posta au Barua Pepe

Waombaji wa ruzuku watawasilisha nakala mbili (2) za maandiko ya miradi yaani nakala ya kielektroniki *(electronic copy*) na nakala ya kine *(hard copy)* kwenye ofisi ya Mfuko wa Misitu Tanzania. Nakala ya kine itawasilishwa kwa njia ya posta na nakala ya kielektroniki itawasilishwa kupitia anwani ya barua pepe ya Mfuko ambayo ni info@forestfund.go.tz , Hata hivyo, nakala ya kielektroniki ni lazima iwe kwenye **muundo wa PDF**.

Maandiko ya miradi yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au barua pepe yataingizwa kwenye mfumo wa **MNRT Portal** na waombaji wa ruzuku watapokea ujumbe kwenye simu zao wa kuwajulisha kuhusu kupokelewa kwa maandiko yao ya miradi. Hivyo, waombaji wote wa ruzuku wanakumbushwa kuandika namba za simu kwenye sehemu ya mawasiliano iliyopo kwenye muundo wa kuandaa maandiko ya miradi.

Maandiko yote ya miradi kwa njia ya posta na barua pepe yaelekezwe kwa:

*Katibu Tawala,*
*Mfuko wa Misitu Tanzania,*
*Jengo la Bodi ya Mfuko wa Barabara,*
*Ghorofa ya Kwanza,*
*S.L.P. 1764,*
***DODOMA.***
*Simu: +255 (0)26 2963290*
*Nukushi: +255 (0)26 2963291*
*baruapepe: info@forestfund.go.tz*
*Tovuti: www.forestfund.go.tz*

## 9.0 UPOKEAJI WA MAANDIKO YA MIRADI

Mwisho wa kupokea maandiko ya miradi inayoomba ruzuku ndogo ni tarehe 30 Juni na 31 Desemba 2021. Aidha, mwisho wa kupokea maandiko ya miradi inayoomba ruzuku ya kati na ruzuku kubwa ni tarehe 31 Machi 2021. **Maombi yoyote yatakayowasilishwa baada ya tarehe ya mwisho ya kupokea maandiko ya miradi hayatashughulikiwa**.

***Kwa maelezo ya ziada tafadhali wasiliana na Katibu Tawala, Mfuko wa Misitu Tanzania kwa kutumia anwani, nukushi au namba za simu zilizotajwa hapo juu.***

## 10.0 KUANDAA MAANDIKO YA MIRADI

Maandiko yote ya miradi yanapaswa kutayarishwa/kuandaliwa kwa kutumia miundo iliyoambatishwa. Maandiko ya miradi yanayoomba ruzuku ndogo yataandaliwa kwa kufuata muundo ulioambatishwa kama **Kiambatisho Na. 1.** Maandiko ya miradi yanayoomba ruzuku ya kati na ruzuku kubwa yataandaliwa kwa kufuata muundo ulioambatishwa kama **Kiambatisho Na. 2.**

Maandiko ya miradi ambayo yataandaliwa bila kufuata miundo iliyotajwa kwenye kipengele namba 10 hapo juu hayatakubaliwa. Maandiko ya miradi yasizidi kurasa 15 ukiondoa viambatisho.

## KIAMBATISHO NA. 1: MUUNDO WA KUANDAA MAANDIKO YA MIRADI KUOMBA RUZUKU NDOGO

**UTANGULIZI**

(i) Kabla ya kujaza sehemu husika, tafadhali soma vigezo na madhumuni ya tangazo la kuitisha maandiko ya miradi ili kuhakiki iwapo mradi wako una sifa za kufikiriwa kupatiwa ruzuku.

(ii) Tafadhali andaa andiko la miradi kwa kufuata muundo na maelekezo yaliyotolewa.

(iii) Maandiko ya miradi yawasilishwe kabla ya mwisho wa saa za kazi (saa 9.00 alasiri) ya tarehe ya mwisho ya kupokea maandiko ya miradi.

(iv) Maandiko ya miradi yawe nadhifu, mepesi kusomeka na yaandaliwe kwa kutumia fonti ya *Arial*, pointi 12 na nafasi kati ya sentensi ni 1.5.

(v) Mwombaji wa ruzuku anapaswa kuainisha idadi ya watekelezaji wa mradi na aoneshe ueledi wao kwenye andiko la mradi ili kuthibitisha uwezo wa kutekeleza mradi ulioombewa ruzuku.

(vi) Mwombaji yeyote mwenye maswali au hoja awasiliane na ofisi ya Mfuko kwa kutumia anwani, nukushi au namba za simu zilizotajwa kwenye tangazo la kuitisha maandiko ya miradi.

1.0 **Taarifa za Msingi Kuhusu Andiko la Mradi**

1.1 Jina la Mradi:..........................................................................................................

1.2 Jina na Anwani ya Mwombaji wa Ruzuku: ……………………………………….…..

.................................................................................................................................

1.3 Jina na anwani ya anayefanya mawasiliano:

.................................................................................................................................

1.4 Mahali Mradi utakapotekelezwa:.............................................................................

1.5 Eneo la kipaumbele la Mfuko wa Misitu Tanzania linaloombewa ruzuku:

................................................................................................................................

1.6 Aina ya Ruzuku:.......................................................................................................

1.7 Aina ya Uwezeshwaji:………………………………………………………………….

1.8 Jumla ya gharama ya Mradi (Shilingi):…………………………………………………

1.9 Kiasi cha fedha kinachoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania (Shilingi):

……………………………………………………………………………………………

1.10: Michango mingine ikiwemo ya hali na mali

……………………………………………………………………………………...…

1.11 Muda wa Utekelezaji wa Mradi na Mwezi ambao Utekelezaji utaanza:

………………………………………………………………………………………………

2. Utangulizi (Usuli wa Mradi):…………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

3. Mantiki na Uthibitisho wa mradi:-……………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………

4. Malengo ya mradi na Viashiria vya utendaji………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

5. Matokeo yatarajiwayo kutoka kwenye mradi:………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

6. Shughuli mahususi zitakazotekelezwa ili kufikia matokeo:…………………………………...

…………………………………………………………………………………………………

7. Watakaonufaika na mradi:…………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

8. Hatua au mbinu zitakazotumika ili kufikia malengo:………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

9. Watakaohusika na utekelezaji wa mradi na ueledi wao. Mwombaji wa ruzuku anapaswa kuainisha idadi ya watekelezaji wa mradi na aoneshe ueledi wao kwenye andiko la mradi ili kurahisisha na kufanikisha utekelezaji wa mradi:

…………………………………………………………………………………………………

10. Ratiba ya utekelezaji wa Mradi:……………………………………………………..………

…………………………………………………………………………………………………..

11. Faida za mradi huu kwa Taifa ni nini? Kwa nini Mfuko wa Misitu wa Tanzania utoe ruzuku kwa mradi huu?

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**12. Bajeti ya Mradi**

Bajeti ifafanuliwe kwa kila kipengele na ioneshe kiasi cha fedha kilichoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania, michango wa wadau wengine, na mchango wa mwombaji wa ruzuku. Aidha, michango ya hali na mali ioneshwe kuwa ni sehemu ya gharama ya mradi. Bajeti inatakiwa kuwa na maelezo yanayoonesha jinsi kila kiasi kilivyokokotolewa.

Vipengele vifuatavyo visioneshwe kwenye bajeti kwani havitagharimiwa na Mfuko: mishahara ya watumishi; vifaa vya ofisi ya mwombaji wa ruzuku; ununuzi wa magari, pikipiki na baiskeli; tuzo na gharama nyingine ambazo hazihusiani moja kwa moja na mradi. Mwombaji wa ruzuku atatakiwa kugawanya bajeti ya mradi wake katika awamu mbili. Hata hivyo, 10% ya fedha za awamu ya pili itabakizwa hadi taarifa ya kukamilisha mradi itakapowasilishwa na kukubalika. Mgawanyo wa fedha za ruzuku ni kama ifuatavyo: 50% (fedha za awamu ya kwanza), 50% kutoa 10% ya fedha itakayobakizwa (fedha za awamu ya pili) na 10% ya fedha za awamu ya pili (fedha itakayobakizwa). Bajeti ya mradi (pamoja na mchanganuo wa kila kipengele) inapaswa kuandaliwa kwa mujibu wa maelekezo yaliyopo kwenye Jedwali namba 1 hapo chini.

**Jedwali Na. 1: Jinsi ua Kuandaa Bajeti ya Mradi**

| Kipengele (Shughuli) | Kipimo (Kizio) | Kiasi | Gharama ya kizio (Sh) | umla ya Gharama (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | Jumla ya Fedha yote | | | |
| | Kiasi kinachoombwa kutoka Mfuko | | | |
| | Michango kutoka kwa wadau wengine | | | |
| | Mchango wa Mwombaji wa Ruzuku | | | |

**13 RIDHAA:** *Kwa waombaji ambao ni Taasisi za Umma watajaza kipengele Na. 13.1 tu. Aidha, waombaji ambao sio Taasisi za Umma watajaza vipengele Na. 13.1, 13.2 na 13.3. Hata hivyo, maandiko ya miradi kutoka shule zote za msingi na sekondari yanapaswa kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Halmashauri (yaani wanapaswa kujaza vipengele Na. 13.1 na 13.3)*

13.1 Maoni na Mapendekezoya Mkuu/Kiongozi wa Kikundi/Taasisi/Asasi:

Maoni:--------------------------------------------------------------------------------------------------

Jina:-----------------------------------------------------------------------------------------------------

Cheo:---------------------------------------------------------------------------------------------------

Muhuri rasmi:------------------------------------------------------------------------------------

Sahihi:------------------------------------------ Tarehe:----------------------------------------------

--

13.2 Maoni na Mapendekezoya Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ambapo Mradi utakatekelezwa.

Maoni:-----------------------------------------------------------------------------------------------

Jina:--------------------------------------------------------------------------------------------------

Cheo:-------------------------------------------------------------------------------------------------

Muhuri rasmi:----------------------------------------------------------------------------------------

Sahihi:------------------------------------------------Tarehe:---------------------------------------

13.3 Maoni na Mapendekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri ambapo mradi utakatekelezwa:

Maoni:-----------------------------------------------------------------------------------------------

Jina:--------------------------------------------------------------------------------------------------

Cheo:-------------------------------------------------------------------------------------------------

Muhuri rasmi:----------------------------------------------------------------------------------------

Saini:------------------------------------------- Tarehe:---------------------------------------------

## 14. VIAMBATISHO

Taarifa zinazotakiwa kuambatishwa kwenye andiko la mradi ni kama ifuatavyo:

i) bao la mantiki;

ii) nakala ya cheti cha usajili wa vikundi/asasi/taasisi (isipokuwa kwa taasisi za serikali);

iii) Waombaji binafsi wawasilishe barua za udhamini kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji anapoishi, Afisa Mtendaji wa Kijiji mradi utakapotekelezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ambapo mradi utakatekelezwa; na

iv) Maandiko yote ya miradi ya utafiti yanapaswa kuonesha mapitio ya makala na taarifa za marejeo, na kila rejeo linatakiwa liwe na majina ya waandishi, jina la jarida, jina la kitabu, namba ya juzuu, namba za kurasa na mwaka wa kuchapishwa.

**KIAMBATISHO NA. 2: MUUNDO WA KUANDAA MAANDIKO YA MIRADI KUOMBA RUZUKU YA KATI NA KUBWA**

**UTANGULIZI**

(i) Kabla ya kujaza sehemu husika, tafadhali soma vigezo na madhumuni ya tangazo la kuitisha maandiko ya miradi ili kuhakiki iwapo mradi wako unazo sifa za kufikiriwa kupatiwa ruzuku.

(ii) Tafadhali andaa andiko la miradi kwa kufuata muundo na maelekezo yaliyotolewa.

(iii) Maandiko ya miradi yawasilishwe kabla ya mwisho wa saa za kazi (saa 9.00 alasiri) ya tarehe ya mwisho ya kupokea maandiko ya miradi.

(iv) Maandiko ya miradi yawe nadhifu, mepesi kusomeka na yaandaliwe kwa kutumia fonti ya *Arial*, pointi 12 na nafasi kati ya sentensi ni 1.5.

(v) Mwombaji wa ruzuku anapaswa kuainisha idadi ya watekelezaji wa mradi na aoneshe ueledi wao kwenye andiko la mradi ili kuthibitisha uwezo wa kutekeleza mradi ulioombewa ruzuku.

(vi) Mwombaji yeyote mwenye maswali au hoja awasiliane na ofisi ya Mfuko kwa kutumia anwani, nukushi au namba za simu zilizotajwa kwenye tangazo la kuitisha maandiko ya miradi.

**1.0 Taarifa za Msingi kuhusu Andiko la Mradi**

1.1 Jina la Mradi: ....................................................................................................................

1.2 Jina na Anwani ya Mwombaji wa Ruzuku:………………………………………………

.............................................................................................................................................

1.3 Jina na Anwani ya Anayefanya Mawasiliano:……………………………………………..

.............................................................................................................................................

1.4 Mahali Mradi utakapotekelezwa :………………………………………………………

.......................................................................................................................................

1.5 Eneo la kipaumbele la Mfuko wa Misitu Tanzania linaloombewa ruzuku: ....................

……………………………………………………………………………………………..

1.6 Aina ya Ruzuku inayoombwa:...........................................................................................

1.7 Aina ya uwezeshwaji unaoombwa:…………………………………………………….…

1.8 Jumla ya gharama ya Mradi (Shilingi):……………………………………………………

1.9 Kiasi cha fedha kinachoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania (Shilingi):

……………………………………………………………………………………………………

1.10 Michango mingine ikiwemo ya hali na mali

…………………………………………………………………………………………….….

1.11 Mantiki na uthibitisho wa kuwa na mradi (yasizidi maneno 250)…………………….…

……………………………………………………………………………………..……

1.12 Malengo ya mradi na viashiria vya utendaji……………………………………….……

……………………………………………………………………………………………..

1.13 Matokeo yanayotarajiwa kutoka kwenye mradi…………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

1.14 Watakaonufaika na Utekelezaji wa mradi……………………………………………..…

……………………………………………………………………………………………..

1.15 Muda wa utekelezaji wa mradi na mwezi ambao utekelezaji utaanza:.......................

……………………………………………………………………………………………..

**2. RIDHAA:** *Kwa waombaji ambao ni Taasisi za Umma watajaza kipengele 2.1. Aidha, waombaji ambao sio Taasisi za Umma watajaza vipengele Na. 2.1, 2.2 na 2.3.*

2.1 Mapendekezo ya Mkuu/Kiongozi wa Taasisi/Kikundi/Asasi inayoomba ruzuku

Maoni:------------------------------------------------------------------------------------------------------

Jina:--------------------------------------------------------------------------------------------------------

Cheo:-------------------------------------------------------------------------------------------------------

Muhuri rasmi:--------------------------------------------------------------------------------------------

Saini:------------------------------------------------------- Tarehe:------------------------------------------

2.2 Mapendekezo ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kata/Mtaa (ambapo mradi utakatekelezwa).

Maoni:------------------------------------------------------------------------------------------------------

Jina:--------------------------------------------------------------------------------------------------------

Cheo:-------------------------------------------------------------------------------------------------------

Muhuri rasmi:--------------------------------------------------------------------------------------------

Saini:------------------------------------------------- Tarehe:-----------------------------------------------

2.3 Mapendekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri ambapo mradi utakatekelezwa:

Maoni:----------------------------------------------------------------------------------------------------

Jina:-------------------------------------------------------------------------------------------------------

Cheo:----------------------------------------------------------------------------------------------------

Muhuri rasmi:-------------------------------------------------------------------------------------------

Saini:---------------------------------------------- Tarehe:---------------------------------------------

## 3.0 ANDIKO

### 3.1 Muhtasari wa Mradi

Muhtasari wa mradi unatakiwa kuwa na sehemu muhimu zote za andiko la mradi ikiwemo kueleza changamoto zilizokufanya kuomba ruzuku, jinsi utekelezaji wa mradi utakavyochangia utatuzi wa changamoto, malengo ya mradi, matokeo yanayotarajiwa kutoka kwenye mradi, shughuli kuu zitakazotekelezwa, matumizi ya matokeo ya mradi katika kuendeleza uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu. Muhtasari usizidi maneno 250 na uoneshe pia bajeti ya mradi na kiasi cha fedha kinachoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania.

### 3.2 Utangulizi

Waombaji wa ruzuku wanapaswa kuelezea kwa kifupi kikundi/asasi/taasisi inayoomba ruzuku ikiwemo tarehe na namba za usajili, kueleza changamoto zilizokufanya kuomba ruzuku, jinsi utekelezaji wa mradi utakavyochangia utatuzi wa changamoto, jitihada zilizokwisha fanywa au zinazoendelea kufanywa katika kuishughulikia changamoto au kutatua changamoto husika.

### 3.3 Azma na Madhumuni ya Mradi na Matokeo Yanayotarajiwa

Mwombaji wa Ruzuku anatakiwa kufafanua azma ya mradi akionesha jinsi utekelezaji wa mradi utakavyochangia uendelezaji wa misitu au kuboresha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu kwenye eneo la utekelezaji wa mradi. Ni muhimu kueleza malengo ya mradi na matokeo yatakayopatikana kutokana na utekelezaji wa mradi. Mwombaji aonyeshe pia jinsi utekelezaji wa mradi unaoombewa ruzuku utakavyoimarisha jitihada za kuboresha maisha ya jamii, ushiriki na ufahamu wao katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu. Mikakati ya kusambaza matokeo ya mradi pia iwekwe wazi. Sehemu hii pia ieleze watakaonufaika wa mradi na jinsi kila mmoja atakavyonufaika na utekelezaji wa mradi. Mwombaji wa ruzuku anatakiwa kuandaa bao la mantiki ambalo kwa lugha ya kiingereza linajulikana kama *Log frame*. Aidha, shughuli za mradi ziainishwe na ratiba ya utekelezaji wa shughuli za mradi (Mpango kazi) inapaswa kuandaliwa ili kusaidia

uperembaji na ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi. Ratiba ya utekelezaji wa shughuli za mradi itasaidia pia katika maandalizi ya bajeti ya mradi.

### 3.4 Mbinu za Kutekeleza Mradi

Katika sehemu hii mwombaji wa ruzuku anatakiwa aweke bayana jinsi anavyotarajia kufanikisha malengo ya mradi na matokeo yanayokusudiwa. Shughuli za mradi zitakazotekelezwa ili kufikia matokeo zielezwe kikamilfu na mpango wa kazi wa shughuli hizo uandaliwe. Aidha, michango ya wadau wengine katika utekelezaji wa mradi ni lazima iwekwe bayana.

### 3.5 Vichocheo vya Mafanikio

Mwombaji wa ruzuku aeleze na kuchambua vichocheo ambavyo vitasaidia kufikia mafanikio ya mradi na vichocheo ambavyo vitaathiri utekelezaji wa mradi. Aidha, mwombaji wa ruzuku aeleze jinsi ya kukabiliana na vichocheo ambavyo vitaathiri utekelezaji wa mradi. Uchambuzi wa vichocheo hivyo unatakiwa utilie maanani muktadha wa mradi mzima na uwezo na ueledi wa watakaohusika na utekelezaji wa mradi.

### 3.6 Mpango wa Uperembaji na Tathmini

Sehemu hii inapaswa kueleza jinsi mradi utakavyofanyiwa uperembaji na tathmini katika kipindi chote cha utekelezaji wake. Kuwepo na maelezo ya vigezo vitakavyotumika kupima iwapo utekelezaji wa shughuli za mradi utaleta mabadiliko kwenye tatizo au utachangia utatuzi wa changamoto ambazo mradi umelenga kuzitatua. Aidha, mwombaji wa ruzuku anapaswa kutoa ufafanuzi unaohusu jinsi ya kupima mafanikio ya mradi. Ni muhimu pia kutambua kuwa bao la mantiki linaloonesha malengo ya mradi, shughuli na matokeo tarajiwa ya mradi linapaswa kutayarishwa ili kusaidia uperembaji na ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi.

### 3.7 Mpango Endelevu wa Mradi

Sehemu hii inapaswa kuelezea jinsi mradi utakavyoendelea kutekelezwa baada ya ukomo wa ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania. Sehemu hii ni muhimu sana na ni vyema ikafahamika kuwa maandiko ya miradi ambayo hayataonesha jinsi mradi utakavyoendelezwa baada ya ukomo wa ruzuku ya Mfuko, hayatapatiwa ruzuku.

### 3,8 Faida za Utekelezaji wa Mradi kwa Taifa

Sehemu hii inapaswa kuelezea jinsi utekelezaji wa mradi utakavyofaidisha Taifa la Tanzania, na uelezee kwa nini Mfuko wa Misitu wa Tanzania utoe ruzuku kwa mradi wako. Hii ni sehemu muhimu ambayo inapaswa kuonesha matokeo fuasi ya mradi *(Project outcomes).*

### 3.9 Bajeti ya Mradi

Bajeti ni sehemu muhimu ya ombi la ruzuku, hivyo bajeti ya mradi inatakiwa:

(i) iwe ina uhalisia na inayokubalika;

(ii) ieleze kila kipengele kikamilifu;

(iii) iwe inaeleweka kirahisi;

(iv) iwe na uhusiano na mpango kazi (ratiba ya utekelezaji wa mradi);

(v) iwe na hesabu sahihi; na

(vi) izingatie ukweli na iwe inaweza kutetewa.

Bajeti ifafanuliwe kwa kila kipengele na ioneshe kiasi cha fedha kilichoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania, michango wa wadau wengine, na mchango wa mwombaji wa ruzuku. Aidha, michango ya hali na mali ioneshwe kuwa ni sehemu ya gharama ya mradi. Bajeti inatakiwa kuwa na maelezo yanayoonesha jinsi kila kiasi kilivyokokotolewa. Vipengele vifuatavyo visioneshwe kwenye bajeti kwani havitagharimiwa na Mfuko: mishahara ya watumishi; vifaa vya ofisi ya mwombaji wa ruzuku; ununuzi wa magari, pikipiki na baiskeli; tuzo na gharama nyingine ambazo hazihusiani moja kwa moja na mradi. Mwombaji wa ruzuku atatakiwa kugawanya bajeti ya mradi wake katika awamu nne za malipo kama ifuatavyo: 40% fedha za awamu ya kwanza, 30% fedha za awamu ya pili, 30% (kutoa 10% ya fedha itakayobakizwa) fedha za awamu ya tatu, na awamu ya nne ni 10% ambayo ni fedha itakayobakizwa kutoka fedha za awamu ya tatu. Bajeti ya mradi (pamoja na mchanganuo wa kila kipengele) imeoneshwa kwenye Jedwali namba 2 hapo chini.

**Jedwali Na. 2: Jinsi ya Kuandaa Bajeti ya Mradi**

| Kipengele (Shughuli) | Kipimo (Kizio) | Kiasi | Gharama ya kizio (Sh) | umla ya Gharama (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | Jumla ya Fedha yote | | | |
| | Kiasi kinachoombwa kutoka Mfuko | | | |
| | Michango kutoka kwa wadau wengine | | | |
| | Mchango wa Mwombaji | | | |

## 4.0 VIAMBATISHO

Taarifa zinazopaswa kuambatishwa kwenye andiko la mradi ni muundo wa asasi/ taasisi/ (isipokuwa kwa Taasisi za Serikali), bao la mantiki, nakala ya cheti cha asajili wa vikundi/asasi/taasisi (isipokuwa kwa Taasisi za Serikali), uthibitisho wa kukubali kushiriki katika utekelezaji wa mradi ukutoka kwa washiriki wa mradi, na wasifu wa watakaohusika na utekelezaji wa mradi. Maandiko yote ya miradi ya utafiti yanapaswa kuonesha mapitio ya makala na taarifa za marejeo na kila rejeo linatakiwa liwe na majina ya waandishi, jina la jarida, jina la kitabu, namba ya juzuu, namba za kurasa na mwaka wa kuchapishwa.